

**CAPITAL MARKETS AND  
SECURITIES AUTHORITY**



**MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI  
NA DHAMANA**

**JIEPUSHE NA MICHEZO YA  
PIRAMIDI "PYRAMID SCHEMES"**

**JIHADHARI NA MIPANGO YA  
KITAPELI**

## Yaliyomo

1.	Nini Maana ya “Pyramid Schemes”.....1
2.	Mfano wa Mlolongo wa Uchangiaji wa Upatu Haramu.....2
3.	Sifa za Upatu Haramu.....3
4.	Tofauti Kati ya Upatu Haramu na Uwekezaji wa Pamoja.....4
5.	Tofauti Kati ya Upatu Haramu na Mipango Mingine .....4
6.	Sheria Inasemaje Kuhusu Upatu Haramu.....5
7.	Aina na Mifano ya Upatu Haramu.....7
8.	Mifano ya Upatu Haramu Iliyowahi Kuchezwa Hapa Nchini .....7
9.	Ushauri kwa Umma.....8
10.	Orodha ya Madalali wa Soko la Hisa la Dar es Salaam.....10
11.	Orodha ya Washauri wa Uwekezaji.....12

## **1. WANANCHI JIHADHARINI NA UPATU HARAMU**

**Katika siku za hivi karibuni** baadhi ya watu wameshawishika kuwekeza katika mipango ijulikanayo kama “pyramid scheme” ambayo inaaahidi faida kubwa ajabu ikilinganishwa na mchango mdogo ambao mwanachama anatakiwa kuchangia.

### **1.1. Nini maana ya “Pyramid Scheme”**

“Pyramid schemes” au upatu haramu ni mpango au mchezo wa kuchangisha fedha unaoendeshwa na mtu au kikundi fulani cha watu kwa kuwadanganya kuwapatia wachangiaji faida kubwa na kwa kipindi kifupi. Mipango hii imekua kivutio kikubwa kwa wachangiaji kutokana na ahadi ya malipo ya faida kubwa na kwa muda mfupi, bila ya wachangiaji kujihusisha kwa namna yoyote na shughuli za uendesahji wa mpango wenyewe.

Ili kushiriki katika “pyramid scheme”, mchangiaji hutakiwa kuchangia kiasi fulani na anatakiwa awashawishi wengine wafanye kama yeye.

Matarajio ni kwamba kila mtu atakuwa na nafasi sawa ya kufikia kilele na kupata malipo kutokana na mchango wa wanachama wengine.

Mpango huu ni wa udanganyifu. Mpango huu hauelezi ni jinsi gani pesa zilizochangwa zinatumiwa kuzalisha faida. Vile vile hakuna mfumo ulioandaliwa wa kuhakikisha kwamba mchango yote iliyokusanywa hutumiwa kwa faida ya wachangiaji.

Mipango ya aina hii huendeshwa kwa namna ambayo fedha za kila mshiriki mpya, hutumiwa kumlipa mshiriki aliyetangulia. Ili kila mshiriki aweze kulipwa, ni lazima wawepo washiriki wengi wapya ambao wana nia na uwezo wa kulipa fedha katika mpango huo. Mara nyingi upatu haramu hufikia mwisho wake pale ambapo wachangiaji zaidi hukosekana.

Kwa mfano tuchukulie kwamba katika mpango mmoja, mchangiaji anatakiwa kuchangia shilingi 50,000/= na kupewa shilingi 300,000 baada ya miezi mitatu. Ili kumlipa mchangiaji wa kwanza, unahitaji wachangiaji 6 katika safu ya Pili. Ili kuwalipa wachangiaji waliolipa katika safu ya Pili, unahitaji wachangiaji 36 katika safu ya tatu. Katika safu ya nne, unahitaji wachangiaji 216. Kwa kila safu imeongezeka

idadi kubwa na wachangiaji wanaohitajika kiasi cha kufanya michango yenyewe isiwe endelevu.

1.2. **Kiambatisho Na: 1** Katika mfano huu, mchangiaji anatoa shilingi 50,000/= na anapewa 300,000/=baada ya miezi 3. Katika safu ya 17, watahitajika wachangiaji wapya 2,821,109,907,456 kuchanga TZS 141,055,495,372,800,000/= ili kuwalipa wachangiaji kwenye safu ya 16. Kwa mfano huu, mchezo huo sio endelevu.

**Jedwali Na: 1**

<b>MFANO WA MLOLONGO WA UCHANGIAJI WA PIRAMIDI</b>			
<b>Kiasi cha kuchangia 50,000</b>			
<b>Ngazi ya Malipo</b>	<b>Wachangiaji wapya</b>	<b>Jumla ya wachangiaji</b>	<b>Kiasi cha Malipo</b>
1	1	1	50,000
2	6	7	300,000
3	36	43	1,800,000
4	216	259	10,800,000
5	1,296	1,555	64,800,000
6	7,776	9,331	388,800,000
7	46,656	55,987	2,332,800,000
8	279,936	335,923	13,996,800,000
9	1,679,616	2,015,539	83,980,800,000
10	10,077,696	12,093,235	503,884,800,000
11	60,466,176	72,559,411	3,023,308,800,000
12	362,797,056	435,356,467	18,139,852,800,000
13	2,176,782,336	2,612,138,803	108,839,116,800,000
14	13,060,694,016	15,672,832,819	653,034,700,800,000
15	78,364,164,096	94,036,996,915	3,918,208,204,800,000
16	470,184,984,576	564,221,981,491	23,509,249,228,800,000
17	2,821,109,907,456	3,385,331,888,947	141,055,495,372,800,000

Katika nchi nyingi michezo ya piramidi imewafanya watu wengi kupoteza akiba zao na baadaye kufilisika na bila ya kuwa na uhakika wanamdai nani ili awafidie hasara waliyoipata. Hapa kwetu mpango huu ni haramu. Mtu au kikundi chochote kinachoanzisha mpango huu anavunja sheria. Vivyo hivyo, mtu yeyote anayechangia kwenye mpango huu pia huvunja sheria.

**2. Sifa za Upatu Haramu**

Utajuaje kwamba huu ni upatu haramu?

1. Huahidi faida kubwa bila kueleza faida hiyo itazalishwaje.

2. Haina waraka wa matarajio kueleza mkakati mzima utafanyikaje.
3. Mchangiaji mpya anahamasishwa awashawishi wachangiaji wengine
4. Mipango hii haina idhini ya Mamlaka husika za Serikali.
5. Waendeshaji wana desturi ya kuonyesha orodha kubwa ya watu mbalimbali na faida kubwa waliyopata kutokana na mpango huo kama kivutio kwa wachangiaji wapya.
6. Hamna mkataba wa kujiunga au kurudishiwa fedha endapo waendeshaji wa mpango hawatatimiza ahadi zao.
7. Katika mipango hii hamna mradi maalum wa kuwekeza fedha hizo wala hamna huduma maalumu itokanayo na uwekezaji wa fedha hizo.
8. Mapato ya mradi huo hutokana na wachangiaji wapya na ada ya kiingilio wanazotozwa wachangiaji.

### **3. Tofauti Kati ya Upatu Haramu na Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja.**

Tofauti na upatu haramu, vyombo vya uwekezaji wa pamoja vina sifa zifuatazo:-

- Fedha zinazochangwa huwekezwa kwa pamoja katika vitega uchumi mbali mbali kama katika mabenki, hisa, majengo ya biashara n.k.
- Mwisho wa mwaka wanachama/wachangiaji hugawana faida kadri ya vipande walivyonunua.
- Meneja wa mfuko anapewa kibali cha kuanzisha na kuendesha mfuko na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana
- Mfuko unakua na mdhamini anayesimamia rasilimali za mfuko na mkaguzi wa hesabu
- Mfuko hutoa waraka wamatarajio – waraka huu una taarifa zote muhimu za jinsi mfuko utakavyoendesha.
- Mdhamini, meneja na mfuko wenyewe husimamiwa na Mamlaka ya masoko ya Mitaji na Dhamana.

### **4. Tofauti Kati ya Upatu Haramu na Mipango Mingine ya Uwekezaji.**

Upatu haramu ni tofauti na mipango mingine ya vikundi ya uwekezaji kama vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) na vyombo vya utoaji wa mikopo midogo midogo (Micro lending)

Vitu vya msingi vya kuangalia na kuainisha upatu haramu na vyombo hivi vingine ni kama ifuatavyo:-

- Katika upatu haramu unapeleka pesa na unapewa pesa. Hakuna uwekezaji au shughuli ya kiuchumi tofauti na vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS). Katika vyama vya kuweka na kukopa unaweka akiba, wewe unakopeshwa mtaji, unarudisha mtaji pole pole kulingana na shughuli ya uchumi unayofanya.
- Katika SACCOS unakua mwanachama na unaweka akiba kidogo kidogo na unakopeshwa kulingana na akiba uliyoweka. Katika upatu haramu unatoa kiasi fulani kama mbegu kwa ahadi ya kuvuna maradufu ya mbegu uliyoweka kwa kipindi kifupi.
- Katika mpango wa mikopo midogo midogo (Micro Finance) unapewa mikopo midogo midogo ambayo unatakiwa kurejesha kidogo kidogo kwa kipindi fulani, ina usimamizi wa miradi, na inatoza riba kubwa kuliko SACCOS kwa kuwa mkopaji haweki dhamana yoyote. Upatu haramu unalipwa mbegu uliyopanda na huhitaji kurejesha faida wala kile ulichovuna.

## **5. Sheria Inasemaje Kuhusu Upatu Haramu**

Tungependa kuwatahadharisha wananchi na wawekezaji kwa ujumla kuwa kushiriki na kuendesha upatu haramu ni hatari na kinyume cha sheria na hakuna nchi yoyote duniani iliyohalalisha mipango hii. Sheria imeweka wazi kabisa kuwa anayeendesha, kushawishi pamoja na yeyote anayeshiriki katika upatu haramu anafanya hivyo kinyume cha sheria na endapo atabainika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Zifuatazo ni sheria zinazokataza kuendesha upatu haramu hapa nchini:-

- Kwa mujibu wa sheria za Kanuni za Adhabu (**Penal Code Cap 16 Sect 171A**) ni kosa la jinai kuendesha, kushawishi watu kushiriki, na kushiriki au kuchangia fedha katika upatu haramu. Kwa mujibu wa sheria hii anayebainika kukiuka sheria ikiwa ni ama kuendesha, kusimamia, kushiriki kwa kuchangia pesa, au kushawishi watu wengine wachangie fedha atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria hii.
- Sheria ya Michezo ya Kubahatisha (**Gaming Board Act 2003 Kifungu 55 kifungu kidogo (1)**). Kadhalika sheria hii inapiga marufuku mtu yeyote kuendesha ama kushiriki upatu haramu.

Kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya 1994, kama ilivyorekebishwa 1997 na kuhusisha taratibu za Vyombo vya Uwekezaji wa pamoja, mtu yeyote anayetangaza ama kwa kukaribisha au kushawishi umma kushiriki katika uwekezaji au kuchangia mtaji ni lazima apate kibali cha Mamlaka kufanya hivyo.

Hali kadhalika kulingana na sheria hiyo, taratibu za utoaji wa Waraka wa Matarajio (Capital Markets Prospectus Requirements Regulations) zinamtaka mtu yeyote anayetaka kutoa dhamana au kukaribisha umma kuchangia mtaji lazima atoe Waraka wa Matarajio (Prospectus) ambao umeidhinishwa na Mamlaka.

Tunapenda ileweke wazi kuwa Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilipitishwa na Bunge letu ili kulinda maslahi ya wawekezaji katika kuepuka vitendo vya watu wadanganyifu. Sheria hii imeweka utaratibu bayana unaolenga kumlinda mwekezaji katika sekta ya masoko ya mitaji na dhamana.

## **6. Aina na Mifano ya Upatu Haramu.**

Kuna aina nyingi za upatu haramu na ifuatayo ni mifano michache:

### **6.1. Barua**

Unaweza kupokea barua ambayo inakuhitaji upeleke dola moja au tano za Kimarekani kwa watu waliotajwa katika barua hiyo na uongeze jina lako katika orodha hiyo. Baadaye unaweza kutakiwa kunakili barua hiyo na kuipeleka kwa watu wengine. Mara nyingi barua hii hutajwa kuwa inatambulika kisheria.

Mlolongo huu wa barua unaweza kuwa ni upatu haramu.

### **6.2. Klabu za "Ndege"**

Katika mpango huu mshiriki hutakiwa kununua tiketi ya ndege ili awe mmojawapo wa abiria katika ndege hiyo pamoja na marubani na wasaidizi wake.

Baada ya "rubani" kukusanya fedha kutoka kwa abiria, huyu "rubani" hujiondoa katika mchezo na "rubani" msaidizi huwa rubani na anawapeleka abiria katika ndege nyingine.

Kila abiria anatakiwa atafute abiria wengine zaidi kwa matumaini ya yeye kuwa rubani.



Hao ambao wanafanikiwa kuwa marubani mwanzo wa mchezo huweza kunufaika lakini abiria wengi zaidi huachwa nyuma kwenye ndege wakati itakapoanguka na watapoteza mitaji yao.

### **6.3. Mipango ya Ponzi/Klabu za Kupeana/Networks**

Vilabu hivi vinaundwa kwa malengo ya kuwalipa washiriki wa kwanza kwa fedha ambazo zitaletwa na washiriki ambao watajiunga baadaye. Kwa kuwa hakuna vyanzo vingine vya fedha zaidi ya michango ya washiriki wapya na kwa sababu idadi ya wanachama wapya hatimaye hutoweka na vilabu hatimaye kufilisika.

### **7. Mifano ya Upatu Haramu iliyowahi kucheza hapa nchini.**

Mipango ya upatu haramu ambayo ilikuwa maarufu na watu wengi kupoteza fedha zao hapa nchini nanchi jirani ni pamoja na ifuatayo:-

- Self Progressive Association ya Steven Kakete
- Dollar Jet
- Women Empowerment
- Development Enterprise for Community Initiative (DECI Kenya)

### **8. Ushauri kwa Umma**

Ikumbukwe kwamba baadhi ya miradi inayoendeshwa hapa nchini imeweza kupata kibali cha kuendesha shughuli fulani halali lakini badala yake ikaanzisha upatu haramu. Mwananchi unashauriwa kwamba kabla hujaingia au kukubali kukaribishwa kushiriki katika mpango wowote fanya yafuatayo:

- Omba waendesha miradi hiyo kukupatia katiba au nyaraka zinazoruhusu kuanzisha na kuendesha mradi huo pamoja na waraka wa matarajio (prospectus)
- Pata uhakika / uthibitisho kutoka mamlaka zinazohusika kwamba mradi huo umeidhinishwa kuchangisha fedha kutoka kwa wananchi.

Endapo unafikiria kujiunga na mradi au utaratibu wowote, JIHADHARI!! Mpango au utaratibu huo unaweza kabisa kuwa si mwingine bali ni upatu haramu. Endapo utajiunga na mpango kama huo, si kwamba utapoteza fedha zako tu bali utakuwa unavunja sheria; na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako.

Kuwa makini na fursa za uwekezaji zinazoahidi kutoa kiwango kikubwa cha faida na mapato katika muda mfupi na bila ya jitihada yoyote

kutoka kwako. Endapo unatilia shaka fursa yoyote ya uwekezaji au ushawishi wowote:-

Toa taarifa kwa vyombo vya usalama na mamlaka husika kama:

Polisi: Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai: Simu. 0732 999154.

Tovuti: [www.policeforce.go.tz](http://www.policeforce.go.tz)

Benki Kuu ya Tanzania: simu (22) 2233000/20

Tovuti: [www.bot-tz.org](http://www.bot-tz.org)

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana: simu (22) 2114959/61

Barua pepe: [info@cmsa-tz.org](mailto:info@cmsa-tz.org)

Tovuti: [www.cms-tz.org](http://www.cms-tz.org)

## ***Kiambatisho 1***

### **ORODHA YA MADALALI WA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM**

#### **1. Rasilimali Ltd.**

Jengo la zamani la TACOSHIL Sokoine Drive, DSM

Simu: +255 22 211 1708

Faksi: +255 22 212 2883

Barua pepe: [rasilimali@africaonline.co.tz](mailto:rasilimali@africaonline.co.tz)

#### **2. Tanzania Securities Ltd.**

Ghorofa ya 7, IPS Building

Mtaa wa Samora na Azikiwe, DSM

Simu: +255 22 211 2807

Faksi: +255 22 211 2809

Barua pepe: [tsl@muchs.ac.tz](mailto:tsl@muchs.ac.tz)

#### **3. Solomon Stock Brokers Ltd.**

Ghorofa ya chini, PPF House

Mtaa wa Samora na Morogoro, DSM

Simu: +255 22 211 2874

Faksi: +255 22 213 1969

Barua pepe: [solomon@intafrica.com](mailto:solomon@intafrica.com)

#### **4. Vertex International Securities Ltd.**

Jengo la Annex – Zambia High Commission

Mtaa wa Sokoine na Ohio, DSM

Simu: +255 22 211 0392

Faksi: +255 22 211 0387

Barua pepe: [vertex@intafrica.com](mailto:vertex@intafrica.com)

**5. Orbit Securities Co. Ltd.**

Ghorofa ya 3, Twiga house

Mtaa wa Samora, DSM

Simu: +255 22 211 1758

Faksi: +255 22 211 3067

Barua pepe: [orbit@orbit.co.tz](mailto:orbit@orbit.co.tz)

**6. Core Securities Co. Ltd.**

Ghorofa ya chini, Twiga house

Mtaa wa Samora, DSM

Tel: +255 22 2123103

Fax: +255 22 2182521

Email: [info@coresecurities.co.tz](mailto:info@coresecurities.co.tz)

**Appendix 2**

**Licensed Investment Advisers (Washauri wa Uwekezaji)**

**1. Orbit Securities Company Limited**

3rd Floor, Twiga House, Samora Avenue

P.O.Box 70254 Dar es Salaam

Tel: 255 (22) 2111758

Fax: 255 (22) 2113067

E-mail: [orbit-sec@raha.com](mailto:orbit-sec@raha.com)

**2. Tanzania Securities Limited**

7th Floor, IPS Building, Samora Avenue / Azikiwe Street

P.O.Box 9821 Dar es Salaam

Tel: 255 (22) 21 12807

Fax: 255 (22) 21 12809

E-mail: [tsl@muchs.ac.tz](mailto:tsl@muchs.ac.tz)

**3. Standard Chartered Bank Tanzania Limited**

International House, Shaaban Robert / Garden Avenue

P.O.Box 9011 Dar es Salaam

Tel: 255 (22) 2122160 / 2122162

Fax: 255 (22) 2122089

**4. Rasilimali Limited**

Tacoshili Building, Sokoine Drive

P.O. Box 9373 Dar es Salaam

Tel: 255 - 22 - 2111711 / 255 (0) 744 777818

Fax: 255 - 22 - 2113438

### **5. Consultants for Resources Evaluation Limited**

Ground Floor, Twiga Building Samora Avenue  
P.o. Box 23227 Dar es Salaam  
Tel: 255 - 22 - 2125147  
Fax: 255 - 22 - 2122562  
Email: core@cats-net.com

### **6. Unit Trust of Tanzania**

3rd Floor, Sukari House Sokoine Drive / Ohio Street  
P.O. Box 14825 Dar es Salaam  
Tel: +255 22 212 250 I / 213 7592/ 212 8460 /61  
Fax: +255 22 21 3 7593  
Email: uwekezaji@utt-tz.org  
Website: www.utt-tz.org

### **7. Ernst & Young Advisory Services**

Utalii House, 36 Laibon Road Oysterbay  
P.O.Box 2475 Dar es Salaam  
Tel: +255 22 266 6853 / 266 7659  
Fax: +255 22 266 6869  
Email: EYAS@tz.ey.comguarantee@raha.com

### **8. Choice Capital Management Company Ltd.**

5<sup>th</sup> Floor, NIC Life House, Wing B Sokoine Drive/ Ohio Street  
P.O. Box 61269 Dar es Salaam  
Tel: +255 22 213 3997  
Website: [www.choicecapitalmanagement.com](http://www.choicecapitalmanagement.com)

### **9. Commercial Bank of Africa (Tanzania) Limited**

Amani Place, Ohio Street,  
P.O. Box 9640, Dar es Salaam  
Tel. +255 22 2130113  
Fax: +255 22 2130116  
E-mail: [info@cba.co.tz](mailto:info@cba.co.tz)  
Website: [www.cba.co.tz](http://www.cba.co.tz)

### **10. FTC Consultants Limited**

2<sup>nd</sup> Floor, Osman Towers Zanaki Street  
P.O. Box 22731 Dar es Salaam  
Tel: +255 22 211 5251 / 2 / 3  
Fax: +255 22 213 0519  
Email: info@mbn.co.tz

### **11. Exim Advisory Services Ltd.**

8<sup>th</sup> Floor, Office Academy Scheme Building, Azikiwe Street  
P.O. Box 3219 Dar es Salaam  
Tel: +255 22 213 4156  
Fax: +255 22 213 4157  
Website: [www.eximadvisoryservices.com](http://www.eximadvisoryservices.com)

**CAPITAL MARKETS AND SECURITIES AUTHORITY**



**MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA**

**Afisa Mtendaji Mkuu**  
**Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana**  
**Ghorofa ya 6, Jengo la PPF Tower,**  
**Makutano ya Mtaa wa Ohio na Garden,**  
**S.L.P. 75713 Dar es Salaam,**  
**Simu: +255 22 2114959 / 61**  
**Faksi: +255 22 2113846**

**Barua pepe: [info@cmsa-tz.org](mailto:info@cmsa-tz.org)**  
**Tovuti: [www.cmsa-tz.org](http://www.cmsa-tz.org)**